JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSOKELO

Namba za simu

Mkuu wa Shule 0758324898
Makamu Mkuu wa Shule 0756944535
Matron/Patron 0753382600/0757242696

Shule ya Sekondari Mwakaleli
S.L.P. 126
Tukuyu

Tarehe .....

KUMB. NA…….....

Mzazi/mlezi wa Mwanafunzi.....
S.L.P.....

Yah: MAELEKEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MWAKALELI HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSOKELO MKOA WA MBEYA KIDATO CHA KWANZA KWA WANAFUNZI WENYE MAHITAJI MAALUMU MWAKA 2023.

UTANGULIZI:

Ninayo furaha kukujulisha kuwa mwanao …… amechaguliwa kujiunga na Shule ya Sekondari Mwakaleli kuanza masomo ya kidato cha kwanza, Shule ipo umbali wa kilomita **35** Mashariki mwa mji wa Tukuyu. Shule itafunguliwa tarehe **09/01/2023**

Usafiri wa basi kutoka Mbeya Mjini unapatikana katika kituo cha mabasi cha Nanenane au Uyole kuelekea Tukuyu Mjini na nauli ni shilingi **4,000/=.** Atashukia kituo cha Katumba kabla ya kufika Tukuyu Mjini. Kutoka Katumba hadi Kandete nauli ni shilingi **5,000/=** na kutoka Kandete hadi shuleni ni shilingi **3,000/=** kwa pikipiki

1. **MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:**

SARE YA SHULE - Anapokuja avae sare ya shule au tracksuit. Hairuhusiwi kabisa mwanafunzi kuwa na nguo za nyumbani akiwa hapa shuleni.

1.2.0. SARE YA SHULE NA MAHITAJI MENGINE

1.2.1. WAVULANA

1. Uje na shati mbili (tetron) nyeupe mikono mifupi (zitakaguliwa).
2. Suruali 2 (Esteem One) moja rangi damu ya mzee na ya pili rangi ya kijivu nyeusi isiyo Nyembamba(modo).
3. Viatu vyeusi vya ngozi jozi mbili (vyenye kamba/gidamu), visivyo na visigino virefu.
4. Soksi rangi nyeupe jozi mbili.
5. Sweta 2 (V – shape)1 rangi ya buluu na 1 damu ya mzee. Ni muhimu Kwa ajili ya baridi.
6. Ni muhimu kuwa na mwamvuli
7. Jaketi rangi nyeusi kwa ajili ya mvua na baridi
8. Tai ya kufunga isiyo na lastic inayofanana na rangi ya suruali husika (Ifike kitovuni).
9. Mwanafunzi wa bweni awe na suruali 2 dark buluu zisivaliwe darasani zinavaliwa muda usiyo wa darasani.

10. T-shirt rangi ya njano inapatikana shuleni.

1.2.2. WASICHANA

1. Sketi 2 (Esteem One) moja rangi damu ya mzee na ya pili iwe kijivu nyeusi (Rinda box),ndefu kufikia kifundo cha mguu au sentimeta 20 kutoka kwenye unyayo, ikiwa fupi hutapokelewa.(zitakaguliwa).
2. Uje na shati mbili tetron rangi nyeupe mikono mifupi (zitakaguliwa).
3. Viatu vyeusi vya ngozi siyo vya plastiki, visivyo na visigino virefu jozi mbili vyenye kamba (gidamu).
4. Soski rangi nyeupe ndefu jozi mbili (zisizo na urembo)
5. Sweta mbili (V- shape)1 rangi ya bluu na 1 damu ya mzee.
6. Ni muhimu kuwa na mwamvuli
7. Hijabu 2 (kwa waislamu.Nyeupe kwa kuvaa darasani na nyeusi kwa kushindia.Hijabu zifunike mabega na zisiwe na urembo.
8. Tai rangi ya sketi husika (ifike kitovuni).
9. Kwa wanafunzi wa bweni,uje na sketi 2 dark blue kwa ajili ya kuzivaa Muda usiyo wa darasani.
10. T-shirt rangi ya njano (zinapatikana shuleni).

1.2.3. SARE ZA MICHEZO (Wote)

1. Track suit moja rangi ya Bluu bahari,kigauni chenye mikono mifupi ragi ya dark bluu.
2. Raba za michezo jozi mbili.
3. T-shirt moja (au zaidi) rangi ya njano – itavaliwa wakati wa michezo na baada ya masomo.

1.2.4. VIFAA VYA KUJA NAVYO SHULENI (wote me na **ke)**

1. Daftari kubwa kumi (10) (counter books 3 quire)
2. Begi la kutunzia vitabu/ daftari
3. Kalamu za kutosha.
4. Faili kwa ajili ya kutunzia FOMU ZA TAARIFA BINAFSI ZA MWANAFUNZI, Zinapatikana shuleni (usilete aina tofauti)
5. Mkebe
6. Godoro ft $2^1/_2$ jipya.
7. Mashuka mawili bluu bahari.
8. Blanketi zito.
9. Jaketi rangi nyeusi kwa ajili ya mvua na baridi.
10. **REAM 1 KWA MUHULA MMOJA-Kwa ajili ya mazoezi na mitihani ya shule.**

NB: Tafadhali soma kwa makini maelekezo / Maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu

1. Mwanafunzi haruhusiwi kuvaa nguo za nyumbani akiwa hapa shuleni
2. Mwanafunzi lazima asajiliwe kwanza utawala ndipo ataruhusiwi kuingia darasani.
3. Vifaa vyote aje navyo siku ya kufungua shule ili vikaguliwe.
4. Shule haitoi huduma ya chakula maalumu kwa wanafunzi wenye matatizo.
5. Mwanafunzi Unatakiwa kuja na **BIMA YA AFYA** au kiasi cha shilingi **6,000/=**kwa ajili ya bima ya afya ya CHF iliyoboreshwa hasa kwa ambao hawana bima ya afya ya taifa NHIF,fedha hizi ni lazima uje nazo kwa ajili ya matibabu yako mwenyewe.

Kuna nafasi ya wanafunzi 20 tu kwa vile hakuna miundombinu inayowafaa wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

KARIBU SANA.

SHABAN DANIEL MWALA

MKUU WA SHULE

SHULE YA SEKONDARI MWAKALELI
SHERIA, TARATIBU NA KANUNI ZA SHULE

1.0. UTANGULIZI

Sheria na taratibu za Shule huwekwa ili zitumike kama mwongozo wa maisha na malezi bora kwa Wanafunzi wanaohusika. Ili kuleta nidhamu inayofaa kwa kujifunza na pia Jumuiya inayohusika iweze kuishi pamoja kwa amani na kushirikiana.

Hivyo kila mwanafunzi aliyekubali kujiunga na shule hii anawajibika kufuata sheria na taratibu za shule hii. Ikiwa wewe ni mwenye kuelewa wajibu wako na uko tayari kutimiza wajibu huo na kama unaelewa **NIA YAKO KUBWA NI KUPATA ELIMU**: Sheria na taratibu hizi utaziona nyepesi kufuata, sheria na taratibu hizi ni za kukusaidia wewe na uongozi wa shule kuweza kutekeleza Majukumu kama jamii moja yenye lengo maalum. Kuvunjwa kwa sheria au kanuni hizi kutachukuliwa kuwa ni utovu wa nidhamu na hatua za kinidhamu zitachukuliwa dhidi ya mvunjaji ili kumrekebisha. Kwa hiyo soma na uzielewe vizuri.

2.0 MIPAKA YA SHULE

(a) Mipaka ya shule ijulikane kama ifuatavyo:

i) Mashariki - Zahanati ya Mission
ii) Kusini/Magharibi - Uzio unaunganisha mission na nyumba ya Mkuu wa Shule kuelekea mto Mwatisi
iii) Kaskazini - Barabara itokayo Mission kwenda Kandete kupitia nyuma ya bweni wavulana
iv) Magharibi-- Mwisho wa kiwanja cha mpira wa Shule

Mwanafunzi anapokuwa shuleni haruhusiwi kwenda nje ya shule bila ruhusa kutoka kwa mwalimu wa zamu ambaye:

(a) Atamwandika kwenye daftari ya ruhusa.
(b) Atampa fomu ya ruhusa

3.0. MAADILI MEMA

(a) Kila mwanafunzi wa shule hii anatakiwa:-

(i) Kufuata sheria na taratibu za shule
(ii) Migomo ni marufuku
(iii) Kuwahi kufika shuleni, kuheshimu walimu, wafanyakazi, viranja wa shule, wazee na wageni.
(iv) Kusimama na kusalimu wakubwa/walimu na wafanyakazi wote wanapopita ama kuongea nao.
(v) Kumheshimu mwanafunzi mwenzako. Ni marufuku kabisa kuoneana hususani Wanafunzi wapya. Mwanafunzi mgeni unapoonewa usisite kutoa taarifa mara moja kwa walimu au uongozi wa shule.

(b) Wanafunzi wasitembelee sehemu zifuatazo bila kibali.

(i) Chumba cha walimu (Staffroom)
(ii) Jikoni
(iii) Ofisi za shule
(iv) Maabara na stoo zote
(v) Nyumba za walimu/wafanyakazi

(c) Mwanafunzi awapo shuleni hatakiwi kutenda mambo yafuatayo:

(i) Kuonyesha kiburi, ubishi na fitina kwa yeyote

(ii) Kunywa pombe, kuvuta sigara na kutumia madawa ya kulevya

(iii) Kutukana au kutumia lugha chafu au matusi, utani mbaya, kukebehiana au uchokozi wowote ule.

(iv) Kuwa na silaha yoyote ile kama vile visu, mapanga, bunduki nk.

(v) Kutembelea bweni la jinsia tofauti.

(vi) Kuingia bweni la jinsia tofauti .

(d) Mwanafunzi anatakiwa kuwa safi wakati wote kwa:

(i) Kuvaa nguo nzuri na vizuri. Tumbukiza shati ndani ya suruali

(ii) Kukata nywele vizuri na kuzichana Mitindo ya rasta, karikiti na pank hairuhusiwi. Vile vile kusuka au kunyoa vipara hakuruhusiwi.

(iii) Kunyoa ndevu, kukata kucha, na kuoga kila siku.

(iv). Kutovaa mapambo kama vile mikufu, heleni, bangiri, shanga, kofia, kupaka rangi kucha, wanja, rangi za midomo, kuvaa pete nk.

(e) Wanafunzi hawaruhusiwi kutembelea sehemu zifuatazo:

(i) Vilabu vya Pombe

(ii) Majumba ya starehe

(iii) Majumba ya kufikia wageni (guest house)

(f) Mwanafunzi anatakiwa kuheshimu bendera ya Taifa, picha za viongozi wa serikali, Nembo ya Taifa, nyimbo za Taifa.

(g) Wanafunzi wa jinsia tofauti hawaruhusiwi kuongea/kukaa sehemu zote za giza na vificho.

4.0. TARATIBU ZA MASOMO

I.Mwanafunzi anatakiwa kuwahi shule inapofungua na kuzingatia mambo yafuatayo:-

(a) Kuingia darasani mapema kabla ya mwalimu

(b) Kusimama na kusalimu mwalimu anapoingia darasani

(c) Kuhudhuria vipindi vyote vilivyopangwa katika ratiba ya darasa lake

(d). Kufanya mazoezi majaribio na mitihani yote inayomhusu

(e) Mwanafunzi atawajibika kujifunza na kuongea kiingereza muda wote awapo Shuleni ikiwa ni pamoja na kutekeleza kanuni ya SPEAK ENGLISH ONLY

(f) Mwanafunzi anyooshe mkono wake juu na asimame wakati wa kuuliza au kujibu maswali.

II. Ikiwa mwalimu hayupo darasani mwanafunzi yampasa.

(a) Kusoma kimya darasani

(b) Kutotembea ovyo darasani

(c) Kutotoka nje ya darasa bila sababu

5.0. UTUNZAJI WA MALI ZA SHULE

I. Mwanafunzi anawajibika kutunza, na kulinda mali ya shule kwa matumizi endelevu ya wanafunzi waliopo na wale watakaokuja baadaye. Hivyo

(a) Viti, madawati, meza vitunzwe mahala pake bila kuvihamisha hamisha. Ni marufuku kuburuza viti, meza au madawati.

(b) Majembe, ndoo, makwanja, mashoka, sululu, sahani, na vikombe vitunzwe na kuwekwa mahali pake.

(c) Madirisha na milango ya vyumba vifungwe wanafunzi wanapoondoka shuleni.

(d) Milango na madirisha visibamizwe ovyo.

(e) Kutochezea miundo mbinu ya umeme kwasababu ni hatari inaweza kusababisha moto hivyo kupoteza mali na uhai.

II.Majengo ya shule yatunzwe kwa:

(a) Kufagia na kudeki sakafu na kutoa buibui ukutani na madirishani.

(b) Kusafisha madirisha na vioo

(c) Kutoandika, kuchora na kubandika maandishi kwenye kuta

(d) Vyoo vitumiwe na kuachwa katika hali ya usafi.

6.0. MICHEZO

Michezo ni muhimu sana kwa afya. Sound mind in sound body,kwa hiyo kila mwanafunzi inampasa:-

(a) Kuwa na sare za michezo

(b) Kushiriki mojawapo ya michezo ya hapa shuleni

(c) Kushiriki katika mashindano ya michezo baina ya shule na timu nyingine

7.0. UTARATIBU WA JIKONI

(i)Mwanafunzi haruhusiwi kuvaa ndala au viatu vya wazi awapo jikoni.

(ii) Kuvaa vitambaa kichwani kwa wasichana isipokuwa hijabu kwa waislam.

(iii) Kuingia jikoni bila sababu ya msingi isipokuwa wanafunzi viongozi wa chakula.

(iv) Kutoa kauli chafu kwa wapishi na viongozi wanafunzi wanaoshughulikia masuala ya jikoni (chakula.

(v)Kutupa ovyo vyakula ndani ya bwalo.

(v) Mwanafunzi haruhusiwi kupiga kelele ovyo ovyo awapo jikoni ni lazima afuate taratibu za jikoni.

8.0. UTARATIBU WA KUTOKA WANAFUNZI (OUTING DAY)

-Mwanafunzi ataruhusiwa kutoka siku ya jumamosi ya mwisho wa mwezi kuanzia saa 2:00 Asubuhi hadi saa 8.00 mchana.

-Mwanafunzi atatakiwa kufika paredi na kuhesabu namba kwa wale wote wanaotegemea kutoka siku hiyo ya Jumamosi ya mwisho wa mwezi.

-Hivyo basi mwanafunzi hataruhusiwa kuwa nje ya shule baada ya muda huo saa 8:00 mchana.

9.0. MAKOSA YANAYOWEZA KUMFUKUZISHA MWANAFUNZI SHULE

i. Kuchochea au kusababisha mgomo
ii. Kuwa na tabia mbaya ya kurudiarudia makossa
iii. Kugoma adhabu halali ya mwalimu au kiranja
iv. Kupiga au kupigana
v. Wizi wa aina yoyote
vi. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya
vii. Kuharibu kwa makusudi mali ya shule
viii. Kudharau alama za taifa yaani bendera, fedha, picha za Rais, mwenge, nembo nk.
ix. Kuoa au kuolewa

x. Kusababisha mimba au kupata mimba
xi. Uasherati
xii. Kubaka/kulawiti/ ushoga/usagaji/kupata mimba au kutoa mimba.
xiii. Kiburi au ukaidi
xiv. Kumiliki simu ya mkononi akiwa shuleni
xv. Kutofanya mitihani ya ndani pamoja na mazoezi
xvi. Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa/utoro
xvii. Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu/walezi na jamii kwa ujumla.
xviii. Kushiriki matendo ya uharifu/siasi na matendo yoyote yanayovunja sheria za nchi.
xix. Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.

…….

SHABAN DANIEL MWALA

MKUU WA SHULE

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
SHULE YA SEKONDARI YA MWAKALELI

FOMU YA KUKUBALI

1.Sehemu ya mwanafunzi

Mimi …….... Ninakubali nafasi niliyopewa Kuingia Kidato cha KWANZA mwaka ……katika shule ya Sekondari ya Mwakaleli na nitafika shuleni bila kuchelewa. Ninaahidi Kwamba nitatii na kuzingatia sheria zote za shule na za nchi. Nitakuwa mwanafunzi mwenye bidii katika masomo na kazi ya Elimu ya kujitegemea.

Anwani yangu ya kudumu ni ……..

……...

……..

2. Sehemu ya Mzazi/Mlezi

Mimi …… ninakubali mtoto wangu …….kuchukua nafasi kuingia shule ya sekondari Mwakaleli kidato cha kwanza mwaka 2023 Ninaahidi kumpatia mahitaji yote ya shule kama ilivyo katika maagizo ya kujiunga na shule. Ninakuhakikishia kuwa nitashirikiana na shule wakati wote kuona kuwa mwanangu anatekeleza wajibu wake kwa shule na Taifa. Anuani yangu ya kudumu ni:

……

…….

..…….....

…….

Simu Na ……..

Iwapo nitapata uhamisho au kubadilisha makazi, ni lazima nitaijulisha shule kwa maandishi.

Sahihi ……Tarehe ……

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA
SHULE YA SEKONDARI MWAKALELI
TAARIFA YA BINAFSI YA MWANAFUNZI

1. Jina kamili ……
2. Tarehe ya kuzaliwa ……..(tarehe, mwezi mwaka)
3. Kabila ……Taifa……
4. Dini na madhehebu ……..
5. Jina la baba ……..Taifa…….
6. Anuani ya baba: ……
7. Kazi ya baba ……
8. Jina la mama ……Kazi yake …….....
9. Wazazi wanaishi pamoja au wametengana……
10. Jina na anuani ya mlezi wako kama si mzazi……. kama ni mlezi uhusiano wako naye……..
11. Wakati wa likizo utakuwa kwa nani na wapi (taja sehemu moja tu utakayokwenda kila wakati na anuani.
12. Nathibitisha kwamba habari zote nilizotoa hapa ni kweli na sahihi.

Sahihi ya mwanafunzi ……Tarehe……

Sahihi ya mzazi/mlezi…… Tarehe …….

TAARIFA BINAFSI

1. Jina kamili kama lilivyotumika darasa la saba .....
2. Dini yako/Dhehebu .....
3. Jina kamili la baba mzazi/mlezi .....
4. Kazi yake .....
5. Anwani kamili ya baba mzazi /mlezi .....
6. Na yake ya simu ya mkononi.....
7. Mahali anakoishi baba mzazi/mlezi: Mkoa .....Wilaya.....
   Tarafa.....Kijiji/Mtaa .....

8. Jina kamili la mama mzazi/mlezi .....
   Kazi yake .....
   Anwani kamili ya baba na mama mzazi/mlezi .....
   Namba ya simu ya mkononi.....

   Mahali anakoishi Mama Mzazi Mlezi:
   Mkoa ……., Wilaya ……., Tarafa……, Kijiji/Mtaa……

9. Majina ya watu wanaoruhusiwa kumtembelea / kumchukua mtoto shuleni

Na	Jina	Mahusiano	Mahali anakoishi	Namba ya Simu
1				
2				
3				
4				
5				

10. Shule za Msingi Nilizosoma

Na	Jina la Shule	Darasa	Mwaka	Mkoa	Wilaya	Kijiji
1						
2						
3						
4						
5						

11. Matokeo ya Mtihani wa Darasa la Saba

Na	Jina la Somo	Daraja
1	Uraia na Maadili / Civic and Moral	
2	Sayansi na Teknolojia / Science and Technology	
3	Kiswahili	
4	English Language	
5	Hisabati / Mathematics	
6	Maarifa ya Jamii na Stadi za kazi / Social Studies	

Nilipata wastani wa …..……..

Tarehe niliyoripoti Mwakaleli Sekondari ni ……..

12. Niwapo hapa shuleni ningependa nijishughulishe na

    1.....

    2.....

    3.....

Mfano:michezo mchezo wa……..…,Kikundi cha utamaduni wa……..au ufundi wa.....

Nakubali kuwa niwapo hapa shuleni nitajihusisha/sitajihusisha na mvulana/msichana yeyote katika maswala ya mapenzi na ninaahidi kuwa nitakuwa mwanafunzi mtiifu kwa walimu,wanafunzi wenzangu na wafanyakazi wasio walimu katika shule hii (kata isiyohusika)

Ee Mwenyezi Mungu naomba unisaidie.

Jina .....Saini .....

Tarehe ……..

THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION

PART A

TO: The medical officer

From

……

……

……

……..

……

……

……

Date…….

Mr/Miss……..(Name in full)

Please examine the above named as to his/her physical and mental fitness for a full time teacher training/secondary education. The examination should include the following categories (1-3) each category or sub-category of which will render the applicant in eligible in case of a defect.

1. Eye – right
2. Hearing
3. Limbs
4. Venereal Diseases
5. Leprosy
6. Epilepsy
7. Neuroses
8. Other serious diseases

PART B: MEDICAL CERTIFICATE: (**To be completed by a Government medical officer)**

I have examined the above named and consider that he is physically fit/unfit and mentally fit/unfit for a full time teacher/secondary education

1. Eye sight
2. Hearing
3. Limbs
4. Speech
5. Venereal diseases
6. Leprosy
7. Epilepsy
8. Neuroses
9. Other serious diseases.

Date……

Signature…….

Station ……

Designation……